**Fomu Na. 1**

# BISMIHI TA'ALAH


**AHLUL-BAIT CENTRE (A.B.C)**

**P.O.BOX 7169**

**TEL:+255(0)756476879**

**0752691258**

**E-mail: ahlulbaytcenter@gmail.com**

**ARUSHA - TANZANIA**


**ASALAMU ALAYKUM,**

**NDUGU……………………………………………………………………………..**

**TAFADHALI REJEA BARUA YAKO YA TAREHE……………………………YA KUOMBA KUJIUNGA NA CHUO CHA AHLUL-BAIT CENTRE.**

**TUNAYO FURAHA KUKUTAARIFU KUWA UMEKUBALIWA KUJIUNGA NA CHUO CHETU CHA AHLUL-BAIT CENTER KATIKA MASOMO YA DINI KWA MUJIBU WA MAFUNDISHO YA AHLUL-BAIT(a.s),CHUO CHETU NI CHA BORDING NA KIKO ARUSHA MAENEO YA NJIRO SHUKA KITUO CHA NALOPA KATA MKONO WA KUSHOTO UKITOKEA MJINI.**

**CHUO KINA MASHARTI(tajwa kwenye fomu namba 2) AMBAYO MWANAFUNZI PAMOJA NA MZAZI WANATAKIWA KUYASOMA KWA MAKINI PAMOJA NA KUTIA SAINI KUONESHA WAMEKUBALIANA NA MASHARTI HUSIKA NA KUA MWANAFUNZI ANA AHIDI KUTII HAYO MASHARTI KWANI IKIWA MWANAFUNZI ATAKIUKA HATUA KALI ZITACHUKULIWA IKIWEMO KUFUKUZWA CHUO.**

**KUTOKANA NA KUWA UMEKUBALIWA HIVYO TUNAOMBA VIAMBATANISHI VIFUATAVYO:**

1. **CHETI CHA KUHITIMU KIDATO CHA NNE AU CHA KUHITIMU ELIMU YA MSINGI AU CHUO (MADRASAH) ULIYOSOMA.**
2. **CHETI CHA KUZALIWA.**
3. **BARUA YA MZAZI AU MLEZI INAYOONYESHA KURIDHIA KWAO WEWE KUJIUNGA NA CHUO CHETU.**
4. **CHETI CHA DAKTARI KIKIAMBATANISHWA NA BARUA YA MWANAFUNZI JUU YA MAELEZO KAMA ANA TATIZO LA KIAFYA LA MUDA MREFU mfano kifafa,macho n.k.**
5. **neti**

**Fomu Na. 2**

**MASHARTI YA KUPOKELEWA KWA MWANAFUNZI**

**Mwanafunzi hatapokelewa kwa maana hata pewa chumba cha kulala ikiwa hatatimiza vitu vifuatavyo na ni lazima avikabidhi idara husika:**

1. **Mwanafunzi lazima aje na nauli ya kurudia nyumbani.**
2. **Mwanafunzi awe na kanzu mbili nyeupe pamoja na kofia mbili.**
3. **Picha nne za paspotisaizi.**
4. **Pesa ya shule tsh 35000/=**

**Kwa ajili ya matumizi binafsi mwanafunzi lazima aje na vifuatavyo;**

1. **Shuka mbili za kutandika pamoja na blanketi**
2. **Mto wa kulalia**
3. **Vyombo vya kulia chakula (sahani,bakuli pamoja na kikombe cha chai)**
4. **Ndoo kwa ajili ya kufulia,vifaa vya usafi(skwiza na fagio refu)**
5. **Vifaa vya mazoezi(raba nyepesi, trakisuti na tisheti)**
6. **Begi la chuma kwa ajili ya kuwekea nguo.**

**Ndugu mwanafunzi utatahiniwa kwa kipindi cha miezi mitatu (3),na ukifeli ndani ya muda huo UTALAZIMIKA KURUDI NYUMBANI.**

**Chuo kitafunguliwa tarehe…05/01/2024**

**WABILLAHI TAWFIQ**

**………………………………………**

**Idara ya kupokea wanafunzi.**

**Ahlul-bait centre(ABC)**

**ARUSHA.**

**Fomu Na. 3**

**MAELEZO YA MUOMBAJI**

1. **Jina kamili la muombaji……………………………………….umri………………………………**
2. **Uraia……………………………….**
3. **Tarehe kamili ya kuzaliwa………………………………………**
4. **Mahali ulipozaliwa pamoja na anuani kamili…………………………………………………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………………………………………………………………**
5. **Umeoa?..........................................................**
6. **Kazi uliyokua ukifanya zamani na ya sasa hivi………………………………………………………………………………**
7. **Kiwango cha elimu yako………………………………………………………………………………**
8. **Tafadhali fafanua malengo yako baada ya kuhitimu masomo katika chuo chetu………………………………………………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………………………………………………………………… ……………………………………….**
9. **Kazi/shughuli za wazazi/walezi wako…………………………………………………………………………**
10. **Je unaishi na wazazi wote wawili?.............................................**
11. **Umekifahamu vipi chuo hiki cha AHULUL-BAIT CENTRE?..........................................................................................................**

    **Mimi ________________________ ninakiri kuwa yote yaliyotajwa hapo juu ni kweli, na nitakuwa mtiifu kwa viongozi na uongozi mzima wa chuo chenu kitukufu, na kwa wanafunzi wenzangu pia.**

    **Saini ya muombaji……………………………………..,**

**UTAMBULISHO**

**Sehemu hii ijazwe na mwalimu mkuu wako wa shule, madrasa,mtendaji kata, au shekhe wa mtaa.**

**Mimi kama (sheikh/mwalimu/ustadh/mtendaji/balozi)___________________________ nakubaliana na maelezo ya muombaji hapo juu kuwa ni kweli na tabia yake ni nzuri na anafaa kujiunga na chuo chenu kitukufu.**

**Saini___________**

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU.**

**Namba ya usajili___________ tarehe ya kujiunga_____________**

**Sababu ya kuacha/kuachishwa masomo____________________________________________________**

**Fomu Na. 4**

**MASHARTI YA NDANI YA CHUO**

**Fomu hii isainiwe na mzazi pamoja na mwanafunzi:**

**Allah s.w.t anasema: ENYI MLIO AMINI TEKELEZENI YALE MLIYOKUBALIANA.**

1. **Sala ya jamaa ni lazima kwa wanafunzi wote na baada ya sala mwanafunzi anapaswa kubaki msikitini kwa ajili ya dua na ziyara n.k.**
2. **Mwanafunzi awapo eneo la chuo analazimika kuongea lugha ya kiarabu tu.**
3. **Mwanafunzi analazimika kufanya usafi eneo lake alilopangiwa.**
4. **Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la chuo siku za masomo na hakuna ruhusa ya aina yoyote isipokuwa kwa mgonjwa anayepelekwa hospitali tu na ruhusa maalumu itatolewa na masuul,badala yake mwanafunzi atapata nafasi ya kutoka siku ya alkhamisi kuanzia saa nane mchana na ijumaa kuanzia baada ya sala ya adhuhuri mpaka mwisho saa kumi na mbili jioni.**
5. **Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria darasani vpindi vyote vilivyoko kwenye ratiba bila kukosa hata kipindi kimoja kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa sita na nusu mchana,na mwanafunzi anapokuwa na udhuru wa ugonjwa analazimika kutoa taarifa kwa masuul muhusika kabla ya vipindi kuanza wailla atachukuliwa sheria maalum.**
6. **Mwanafunzi akipata chini ya alama 50% katika masomo matatu atafukuzwa chuoni.**
7. **Wanafunzi hawaruhusiwi kukaa vigenge visivyo na faida,na kukaa maeneo yasiyo wafaa kama getini na vyumba visivyokuwa vyao kwa lengo la kupiga zogo tu.**
8. **Mwanafunzi anatakiwa kujipamba na tabia njema, kama vile kujiheshimu yeye mwenyewe na kuwaheshimu wenzake na pia kuwaheshimu walimu wake wote,na dharau yoyote itakayofanywa na mwanafunzi dhidi ya mwalimu hatua ya kinidhamu itachukuliwa.**
9. **Mwanafunzi analazimika kutunza na kutumia vifaa vya chuo kwa uangalifu kama vile viti,meza,chaki,vitabu,vifaa vya usafi na bila kuharibu hata kimoja vinginevyo atachukuliwa hatua.**
10. **Mwanafunzi analazimika kula chakula ndani ya darning hall {ukumbi wa kulia chakula},na haruhusiwi kabisa kula nje ya hapo.**
11. **Wanafunzi hawaruhusiwi kuja na simu au redio na kama atakamatwa nayo hatua ya kwanza atanyang'anywa na kutorudishiwa kisha hatua kali ya kikanuni itafuatia kama vile kufukuzwa n.k.**
12. **Mwanafunzi haruhusiwi kupokea mgeni yeyote wa jinsia ya kike ila ikithibiti kuwa ni mama yake au dada yake,vile vile haruhusiwi kumlaza mgeni yeyote katika mabweni ya wanafunzi.**
13. **Masomo ya ziada nje,kufundisha nje,haviruhusiwi.**
14. **Vazi la kaptula,kubaki kifua wazi na mengineyo yaliyo kinyume na utaratibu wa kiislamu haviruhusiwi.**
15. **mwanafunzi haruhusiwi kuwa na ukaribu wa ziada na wafanyakazi wa chuo.**

**Jina la mwanafunzi________________________________**

**Saini yake_________________________________**

**Saini ya mzazi/mlezi_________________________**

**Saini ya masuul idara ya masomo____________**

**Tarehe _____________________________**